



OFISI YA WAZIRI MKUU

KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

MRADI WA KUKUZA AJIRA NA UJUZI – TANZANIA

(EMPLOYMENT AND SKILLS FOR EMPLOYMENT – TANZANIA (E4DT))

TAARIFA KWA UMMA

FURSA YA MAFUNZO YA UKUZAJI UJUZI KATIKA FANI ZA UCHOMELEAJI VYUMA VIWANDANI, UFUNDI BOMBA WA VIWANDANI, UFUNDI BOMBA WA MAJUMBANI NA MEKATRONIKI.

1. **Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu** inashirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kutekeleza mradi wa kukuza Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo ya Afrika (E4D). Katika mwaka huu wa fedha Ofisi imepanga kutoa mafunzo ya ujuzi katika fani za Uchomeleaji vyuma viwandani (Industrial Welding), ufundi Bomba wa viwandani (Industrial plumbing), ufundi bomba wa majumbani (domestic plumbing), Mekatroniki (mechatronics) kwa vijana 2,500 wenye umri kati miaka 15 hadi 35. Mafunzo haya yatatolewa na VETA kwa mfumo nadharia na vitendo.
2. Mradi wa E4D unafadhiliwa na Wizara ya Shirikisho la Ujerumani ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo wa Norway (Norad), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Korea ya Kusini (KOICA).
3. Mafunzo yatatolewa katika vyuo vya VETA vifuatavyo:



Implemented by:



Jointly funded by:





- VETA Dodoma - fani za Uchomeleaji wa Viwandani (Industrial Welding), Ufundi wa Bomba viwandani (Industrial plumbing), na ufundi bomba majumbani (Domestic Plumbing)
- VETA Lindi - fani za Uchomeleaji wa Viwandani (Industrial Welding), Ufundi wa Bomba viwandani (Industrial plumbing), na ufundi bomba majumbani (Domestic Plumbing)
- VETA Manyara RVTSC - fani za Uchomeleaji wa Viwandani (Industrial Welding), Ufundi wa Bomba viwandani (industrial plumbing), ufundi bomba wa majumbani (Domestic Plumbing)
- Chuo cha Tehama VETA Kipawa Chuo cha Tehama – Mekatroniki (Mechatronics)
- VETA Gorowa - Ufundi bomba wa majumbani
- VETA Singida - Kozi ya kuchomelea na kuunda vyuma na ufundi bomba wa Majumbani
- VETA Mikumi - Kozi ya kuchomelea na kuunda vyuma na ufundi bomba wa majumbani
- VETA Dakawa - Ufundi bomba wa majumbani
- VETA Iringa - Kozi ya kuchomelea na kuunda vyuma

Baada ya mafunzo ya nadharia na vitendo vyuoni, wanafunzi watakaofuzu watapata fursa ya kufanya mafunzo ya vitendo viwandani chini ya uangalizi wa ATE an GOPA.

4. Vigezo vya kujiunga na mafunzo ni vifuatavyo:

- a) Awe raia wa Tanzania.
- b) Awe na umri kati ya miaka 15 hadi 35 (Idhini ya maandishi ya wazazi/walezi inahitajika kwa waombaji kati ya umri wa miaka 15 hadi 18 wakati wa mafunzo ya vitendo viwandani.)
- c) Awe anaweza kufika katika moja ya vyuo vya mafunzo vya VETA kama vilivyoorodheshwa hapo juu au muda wote wa mafunzo.
- d) Kwa kozi za ufundi bomba viwandani na mekatroniki, mwombaji awe na ujuzi au uzoefu wa walau mwaka mmoja

5. Waombaji wanapaswa kuchukua fomu za maombi katika vyuo vya VETA Dodoma, VETA Manyara, VETA Lindi, na Kituo cha Tehama VETA Kipawa. Waombaji wanaweza pia kupakua na kujaza fomu kupitia tovuti www.veta.go.tz na www.kazi.go.tz

- a) Mzazi/mlezi awe tayari kugharamia mahitaji ambayo hayatafadhiliwa na mradi wakati wa kufanya mafunzo kwa vitendo vyuoni.



Implemented by:



Jointly funded by:





- b) Gharama za kuendesha mafunzo zitalipwa na mradi kwa ajili ya waombaji watakaochaguliwa kujiunga na mafunzo.
 - c) Muda wa kutuma maombi utafunguliwa tarehe 8 Novemba hadi 13 Novemba 2022.
 - d) Mwombaji atatakiwa kuwasilisha viambatanisho vifuatavyo wakati wa kushiriki mafunzo chuoni.
 - i. Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Taifa au kadi ya mpiga kura au barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa anakoishi mwombaji (lazima);
 - ii. Anwani ya makazi, nambari za simu na barua pepe (ikiwa inapatikana).
6. Washiriki watakaochaguliwa watajulishwa kwa njia za barua pepe, SMS, tovuti za chuo husika cha VETA na Ofisi ya Waziri Mkuu (OWM-KVAU) kuanzia 14 - 19 Novemba, 2022. Mafunzo yanatarajiwa kuanza rasmi 21 Novemba, 2022.
7. Tarehe ya mafunzo kwa vitendo viwandani itatangazwa moja kwa moja kwa mwanafunzi aliyechaguliwa na itafanyika katika chuo cha VETA ambako mshiriki ameandikishwa.

Kwa ajili ya kupata taarifa zaidi wasiliana na VETA Makao Makuu, S.L.P 802, Dodoma au barua info@veta.go.tz au simu nambari +255 755 267489.

Imetolewa na:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na
Wenye Ulemavu,
SLP 2890,
Dodoma.
ps@kazi.go.tz

Mkurugenzi Mkazi,
Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ),
SLP 1519,
Dar es Salaam.
giz-tanzania@giz.de



Implemented by:



Jointly funded by:





Implemented by:



Jointly funded by:

